



Familia ya Inzawu ilikuwa yenye furaha. Binti wao wawili walijifunza kutoka kwa mama yao jinsi ya kupika na kutunza bustani.




Kila walipokula chakula cha jioni, waliongea kuhusu waliyotenda siku hiyo.




Baba aliwaonya wanawe kutoingia msituni kabisa. Aliwaambia kuhusu kiumbe cha ajabu kilichoishi katika msitu huo. Alisema, "Kiumbe hicho ni kama sisi wawili pamoja!"




Siku moja, wasichana wale walikuwa wakicheza karibu na mto. Waliuzunguka mti, na ghafla, walikabiliana na kiumbe cha ajabu! Kiumbe hicho kilikuwa na macho mawili, mapua mawili, viganja viwili na mikono miwili.




Wakitetemeka kwa woga, walikimbia kuwaeleza ndugu zao walichokuwa wameona. Hata hivyo, wavulana hao hawakuwaamini, "Ni ujinga wa wasichana tu!" Walisema.




Mwishowe, hamu iliwazidi. Wavulana hao waliwafuata dada zao wakaelekea mtoni ili kujionea wenyewe kiumbe hicho cha ajabu.



Walitafuta na kutafuta lakini waliona nyasi ndefu na miti peke yake. Waliposikia kelele, walitazama juu.




Juu ya mti walikiona kiumbe cha ajabu wasichokuwa wameona tangu. Kilikuwa na macho mawili, mapua mawili, viganja viwili na mikono miwili. Kila sehemu ya mwili ilikuwa mbili mbili kinyume na wao waliokuwa na kimoja pekee.



Watoto hao waliogopa, wakakimbia kuwaambia wazazi wao. Muda mfupi baadaye, familia nzima ilikuwa pale mtoni kukichunguza kiumbe hicho cha ajabu.



"Msiniumize!" Kiumbe hicho kilisema, huku kikijificha nyuma ya mti. Wakati huo, familia ya Inzawu iliweza kuona mguu mmoja, kiganja kimoja, mkono mmoja na jicho moja pekee.



"Mimi ni kama ninyi tu," kiumbe hicho kiliendelea kusema. "Tofauti kati yangu nanyi ni kwamba niliumbwa na mbili mbili ya kila sehemu ya mwili."



Hivyo ndivyo familia ya Inzawu iligundua kwamba kiumbe hicho hakikuwa cha kuogopwa. Ilikuwa tu hali iliyokuwa tofauti na yao.